MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI NA UONGOZI




# SAFARI YETU: Tulikotoka, Tulipo, na Tunakokwenda

MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI NA UONGOZI

# SAFARI YETU:

# Tulikotoka, Tulipo, na Tunakokwenda.

WOMEN FUND TANZANIA TRUST

Empowering Local Women Heroes

**Prepared by:**

Women Fund Tanzania (WFT)

Empowering Local Women Heroes

www.wft.or.tz

@womenfund_tz

# Table of Contents


**1.0 Utangulizi:** Sisi ni Nani? Tumetoka wapi? Tuko wapi? Matarijio yetu ni yapi 02

Maudhui ya Kuundwa kwa Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi 02

Mikakati Iliyotumika 05

Mafanikio 06

Changamoto Kuu za Mchakato wakati wa Kutayarisha Katiba 07

**2.0 Safari Yetu:** Safari ya Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi Tangu 2014 hadi 2024 08

Shughuli zilizotekelezwa na Mtandao tangu 2014 hadi 2024 09

Mgawanyo wa kazi kimashirika ulikuwa kama ifuatavyo 10

Kuimarisha/ujenzi wa Tapo la Utetezi wa Haki za Wanawake 11

Uchambuzi wa Sheria za Uchaguzi 12

Kushinikiza Kusitishwa kwa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Kupambana na Rushwa Ya Ngono 15

Sheria ya Ndoa vifungu vinavyoruhusu Ndoa za Utotoni 22

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kuhusu likizo ya Uzazi kwa Wanawake wenye kujifungua Watoto Njti 23

**3.0 Hitimisho** 24

Tuko Wapi? Mafanikio yapi ? Changamoto zipi? Na Mfunzo yapi 24

Mafanikio ya jumla 24

Changamoto 26

Mfunzo Yatokanayo na Safari Yetu 27

Matarajio Yetu Yatokanayo na mafunzo ya Safari yetu. 27

# Mtandao wanawake, Katiba, Uchaguzi, na Uongozi



# 1.0 UTANGULIZI

**Sisi ni Nani? Tumetoka wapi? Tuko wapi? Matarijio yetu ni yapi.**

## 1.1 MAUDHUI YA KUUNDWA KWA MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UONGOZI NA UCHAGUZI.

Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi ulianzishwa kwanza kama Mtandao wa Wanawake na Katiba, ukiwa na asasi za kiraia zaidi ya 65 mwaka 2011 wakati Rais wa awamu ya Nne, Mh. Jakaya Kikwete alipotangaza nia ya kuanza mchakato wa kutayarisha Katiba Mpya.

Mtandao huu ulitokana na vuguvugu la tapo lililojikita katika kuhakikisha kuwa mchakato na maudhui ya Katiba iliyokuwa inaandaliwa haiachi nyuma ushiriki na sauti za wanawake na wasichana, haswa kwa wale walio wengi na pembezoni. Hivyo basi, ikiwa ni mwendelezo wa kupigania haki na ajenda ya ukombozi wao wa kimapinduzi, wanawake na vijana wa kike kutoka pande mbali mbali za nchi, walikubali kuvunja mipaka inayowazunguka ikiwa ni ya: kijamii, kiuchumi, kidini, kisiasa na kiitikadi, kiumri na kimaumbile, na kuunganisha nguvu zao kwa pamoja kwa kupitia Mtandao huu.

Katika kufanya hivyo, Mtandao huu uliwawezesha wanawake, vijana wa kike nchini kutekeleza mikakati mingi. Mikakati hii ilijumuisha kutafakari na ujenzi wa ajenda ya Mtandao ambayo ilibeba madai ya misingi ya kikatiba kwa wanawake; ujenzi wa muundo wa Mtandao utakaowezesha Tapo kutandaa na umiliki wa pamoja wa ajenda; ujenzi wa mikakati ya mafunzo ya Wanamtandao na wadau mbalimbali; utetezi na ushawishi wa ajenda hiyo katika ngazi mbalimbali, na kuratibu na kutafuta rasilimali watu, fedha na ujuzi kwa kuendesha shughuli za kila siku za Mtandao. Dhumuni la kuunda Mtandao huu ni kushinikiza mchakato wa katiba mpya yenye mrengo wa Jinsia.



Katiba yenye mrengo wa jinsia ni katiba itakayobainisha misingi ya kulinda haki za wanawake, na watoto wa kike. Vile vile ni katiba itakayobainisha misingi itakayoongoza vyombo, vya utawala viwajibike kwa wanawake na wanaume wa Tanzania, kuweka misingi ya utawala wa sheria wenye mtazamo wa jinsia, pamoja na kuweka misingi ya kuwezesha ushiriki wa wanawake na wanaume katika ngazi zote za maamuzi katika taifa letu.

Mchakato wa kutayarisha Katiba yenye mrengo wa Jinsia sharti ujengeke kwenye uelewa kwamba mapengo ya jinsia yanayosababisha haki na stahiki tofauti kati ya wanawake na wanaume zina athari hasi katika kuendeleza taifa hili na zaidi zinaashiria kumbebesha mwanamke kazi kubwa zaidi katika kuendeleza taifa na hapo hapo kumnyima stahiki zake kama binadamu. Utambuzi huu uongoze utayarishaji wa katiba yenye kujenga misingi ya kuondoa tofauti zilizompokonya mwanamke haki na kumbebesha mzigo mkubwa wa kuliendeleza taifa bila nyenzo za kumwezesha kufanya hivyo. Sambamba na haya yote, kuwepo na dhamira ya kubomoa mifumo inayomkandamiza mwanamke, msichana na hata wanaume walioko pembezoni.

Kwa mantiki hii, katiba inayojenga misingi ya usawa na uhuru, katika muktadha wa demokrasia pana, haina budi kuweka misingi ambayo haitaruhusu vipengele vitakavyowapokonya wanawake, au wanaume haki ya kuwa huru na sawa (clawaback clauses). Hii ni katiba iliyotokana na mchakato uliyoshirikisha sauti za wanawake na wanaume katika mchakato wote wa kutayarisha katiba hiyo. Vile vile ni katiba itakayomilikiwa na wanawake na wanaume, hivyo sharti iwekwe kwenye lugha nyepesi itakayowawezesha wanawake kuitumia katika kulinda, kuteteana kudai haki zao.Vile vile ni katiba yenye kuweka msingi itakayoruhusu na kuwajibisha vyombo vya dola kuchukua hatua za makusudi za kurekebisha mapengo yaliyotokana na mfumo wa ubaguzi wa jinsia.

Katiba hii ni lazima iweke bayana makubaliano ya muafaka wa kitaifa yatakayopewa ridhaa na wanawake na wanaume kwa pamoja. Kwamba, katiba mpya sharti ijengewa misingi ya usawa, utu na inayokataza aina zozote za ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia. Ni katiba itakayobatilisha sheria zote zinazokinzana na misingi ya haki na usawa wa jinsia. Hivyo katiba iwajibishe serikali kuhakikisha raia wote, wanawake na wanaume wanapata haki sawa na zinalindwa, na kuna vyombo vya kusimamia ulinzi wa haki hizo.



**Picha**: Kundi la watu wenye mahitaji maalumu wakishiriki kwenye moja ya makongamano ya Mtandao

Kwa kuongozwa na misingi ya hoja hizi, Mtandao wa Wanawake na Katiba ulibainisha maeneo 12 ya kuingiza kwenye Katiba Mpya huku wakibaliana kwa sauti moja kwamba, Wanawake wa Tanzania wanataka Katiba yenye Mrengo wa Jinsia. Maswala hayo ni:

01 Haki za wanawake zibainishwa kwenye katiba

02 Katiba ibatilishe Sheria zote, miongozo na vitendo vyote vyenye kuashiria kumbagua mwanamke.

03 Haki ya utu wa mwanamke vilindwe na utambuliwa kikatiba.

04 Mikataba, itifaki na matamko yote ya kimataifa na kikanda inayobainisha haki za mwanamke yaheshime na kutafsiriwa katika sheria za nchi.

05 Katiba itamke na kutambua haki sawa za wanawake katika ushiriki wao kweniye Nyanja mbalimbali za uongozi.

06 Katiba ibainishe umri wa mtoto wa kuolewa ili kuwalinda hususani watoto wa kike dhidi ya ndoa za utotoni.

07 Haki za wanawake, kufikia, kutumia na hatimaye kumiliki rasimili za nchi zibainishwe kikatiba.

08 Haki za wanawake za kufikia huduma za afya ya uzazi zibainishwe.

09 Haki za wanawake kufikia na kunufaika na huduma za jamii zibainishwe kikatiba.

10 Haki za wanawake wenye ulemavu zibainishwa kikatiba.

11 Kuundwe chombo maalum, au kamisheni ya kushughulikia haki za wanawake ili kuweka mfumo wa uwajibikaji wa utekelezaji wa haki hizi za kikatiba

12 Mhakama ya familia









## 1.2 MIKAKATI ILIYOTUMIKA

Mtandao huu ulitumia mbinu na mikakati mingi katika kushinikiza mchakato wa Katiba Mpya kuwa na mrengo wa jinsia. Kwanza kabisa ni uchambuzi yakinifu wa Katiba iliyokuwepo ili kubainisha na kukubaliana kwa pamoja mapengo yaliyokuwepo, kujenga uelewa wa pamoja wa umuhimu wa kuwa na katiba yenye mrengo wa jinsia, kujenga ajenda ya pamoja. Mtandao uliweza kutumia mikakati shirikishi na ya kimapinduzi ambayo ilifanikisha kuungwa mkono kwa ajenda yao na wadau kutoka sekta mbalimbali wakiwemo wanaume wabunge na wengine.

Vile vile Mtandao ulitumia mkakati wa kujengeana uwezo wa kuielewa dhana nzima ya katiba yenye mrengo wa jinsia. Mbinu hii ilitumia mkakati wa mafunzo ya pamoja, uchambuzi wa katiba nyingine kupata mafunzo, na kukubaliana ajenda ya pamoja ya Mtandao huu katika makongamano na mikutano ya pamoja.

Mikakati ya kuelimisha jamii nzima ya Kitanzania kuhusu umuhimu wa Katiba yenye mrengo wa jinsia ulitumika pia. Njia mbalimbali zilitumika ikiwa ni pamoja na vipeperushi, maongezi ya ana kwa ana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wabunge, viongozi katika ngazi mbalimbali za kijamii, ikiwa ni pamoja na viongozi wa dini, viongozi wa kisiasa, na wanajamii kwa ujumla.

Vile vile Mtandao ulishiriki kwenye kupendekeza wawakilishi wao kwenye Bunge la Katiba, na kushinikiza kuwepo na usawa wa jinsia katika kuongoza mchakato wa Bunge la Katiba.[1] Hatimaye, wanamtandao waliwasilisha mapendekezo yao kwa Tume iliyohusika na uratibu wa zoezi zima la kutayarisha katiba mpya, iliyojulikana kwa jina la Tume ya Warioba ambaye ndiye aliingoza mchakato wote wa uratibu wa mapendekezo ya wanajamii. Katika kupokea madai ya Mtandao wa Wanawake na Katiba, Mh. Warioba alikiri "Hakika hakuna kundi lililokuwa limejipanga kama kundi hili la Wanawake" na Kwamba angalitamani makundi mengine yangejifunza kutoka kwa Mtandao huu.

**"Hakika hakuna kundi lililokuwa limejipanga kama kundi hili la Wanawake"**

**-Mh. Warioba**




**Picha**: Moja ya mikutano na vyombo vya habari kuhamasisha umuhimu wa katiba yenye mrengo wa jinsia

[1] Ushawishi huu ulipelekea kuteuliwa Mh. Suluhu Hassan kuwa makamo wa Mwenyekiti wa Bunge la Katiba jambo ambalo lilipelekea Chama chake kumteua baadaye kama Mgombea mwenza baada ya kuona uwezo wake wa kuliongoza Bunge la Katiba.


## 1.3 MAFANIKIO

Kwanza kabisa ni kuingizwa kwa madai yetu kwenye katiba pendekezwa. Kati ya madai 12 yaliyotajwa hapo awali, tulifanikisha kuingizwa kwa madai 11 na nusu. Suala la kuwa na chombo maalum cha kushuhgulikia uzingatiaji na ua utekelezwaji wa madai lilikubalika lakini Tume ikashauri suala hilo liliingizwe kwenye hadidu rejea za Tume ya Haki za Binadamu. Fanikio lingine kubwa ni kuimarika kwa tapo liloweza kujenga sauti ya pamoja, ajenda moja, katika kushinikiza kuwepo kwa katiba yenye mrengo wa jinsia.

Sambamba na hili ni utambuzi wa nguvu zetu wanawake na wasichana katika kudai haki na katika kuwezesha kufanikisha madai yetu. Vile vile ni ule uwezo wa kuunganisha makundi mbalimbali kuwa na umiliki wa ajenda ya pamoja kuhusu haki za kikatiba wanazozidai katika muktadha ulioashiria kugawanya wanawake katika makundi mengi yakiwemo ya: tabaka za kiuchumi, umri, dini, itikadi za kisiasa, makazi na tabaka nyingine nyingi.

Matumizi ya mikakati shirikishi iliyoweza kushawishi kuungwa mkono kwa ajenda yetu na wadau mbalimbali wakiwemo wanaume viongozi katika ngazi mbalimbali za kijamii, dini, siasa waliokuwa na fikra za kimapinduzi kukubaliana na ajenda yetu na kuiteteana kushawishi wengine kuikubali ni moja ya fanikio la mtandao.

Umiliki wa ajenda na wadau wote watetezi wa haki za wanawake na watoto ni fanikio kubwa na funzo kubwa kutokana na mchakato huu. Kuendeshwa kwa shughuli za Mtandao kwa kutegemea zaidi rasilimali na nguvu za wanaMtandao katika ngazi mbalimbali ni fanikio kubwa na ni mkakati wa kuendelezwa, kwani unaondoa dhana ya kuwa ujenzi wa Tapo ulio na matokeo endelevu hauwezekani bila ya kutegemea zaidi rasilimalina nguvu ya nje ya tapo hilo Kimantiki, Mtandao wa Wanawake na Katiba ulifanikisha kwa kiasi kikubwa azma yake ya kuingizwa kwa masuala kumi na moja kati ya kumi na mawili kwenye Katiba Pendekezwa na hivyo kuwa na rasimu ya Katiba iliyokuwa na Mrengo wa Jinsia.




**Mafanikio:**
**Kati ya madai 12 yaliyotajwa hapo awali, tulifanikisha kuingizwa kwa madai 11 na nusu.**

## 1.4 CHANGAMOTO KUU ZA MCHAKATO WAKATI WA KUTAYARISHA KATIBA

Changamoto kubwa ni kusitishwa kwa mchakato wa kuwepo kwa katiba mpya baada ya kuahirisha au kusitisha kabisa mchakato wa kura ya maoni. Hali hii imejenga wasiwasi mkubwa kwa wanamtandao kuhusu uwezekano wa kupoteza mafanikio yaliyotokana na mchakato wa kutayarisha rasimu ya Katiba Mpya.

Sambamba na hili, ni kushindwa kujenga muafaka na umoja wa Kitaifa kuhusu misingi ya kikatiba ambayo haiyumbishwi na tofauti za kiitikadi, kidini, kijinsi na wala kitabaka. Katika nchi zinazoongozwa na misingi ya demokrasia shirikishi yenye mrengo wa jinsia, katiba ikiwa ni sheria mama, hubainisha misingi mikuu itakayoongoza taratibu zote za utunzi wa sheria, haki za kila mtu ikiwa ni pamoja na ushiriki wa raia wote (Ke na Me ) katika meza ya maamuzi. Hivyo basi, kusitishwa kwa mchakato wa kutayarisha misingi mipya ya kuongoza taifa letu, ni hatarishi kwa ujenzi wa demokrasia shirikishi na yenye mrengo wa jinsia hapa nchini.

Pamoja na changamoto tajwa, wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi hawakukata tamaa. Sehemu ya Pili inayofuata tutaelezea kwa kifupi safari ya Mtandao tangu 2014 hadi leo hii.




**Changamoto:**

- **Kusitishwa kwa mchakato wa kuwepo kwa katiba mpya baada ya kuahirisha au kusitisha kabisa mchakato wa kura ya maoni**
- **Kushindwa kujenga muafaka na umoja wa Kitaifa kuhusu misingi ya kikatiba ambayo haiyumbishwi na tofauti za kiitikadi, kidini, kijinsi na wala kitabaka.**

# 2.0 SAFARI YETU

## Safari ya Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi Tangu 2014 hadi 2024

Katika kipindi cha takribani miaka kumi tangu kuahirishwa zoezi la kutayarisha katiba mpya Wanamtandao wa Wanawake na Katiba, walijiongezea hadidu rejea mpya ya Uchaguzi na Uongozi, hivyo Mtandao ukajulikana kama "Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi".

Baada ya tafukuri ya kina, wa katiba pamoja na sheria mbalimbali, wanamtandao walikubaliana kuendelea kushawishi na kushinikiza mabadiliko katika baadhi ya sheria zetu ikiwa ni pamoja na maboresho ya katiba iliyoko ili kuboresha au kuondoa vipengele vilivyohalalisha ubaguguzi kinyume na msingi iliyobainishwa na kukubaliwa na nchi, katika mikataba ya Kimataifa, Kikanda ambayo nchi yetu imerithia na hata kwenye katiba iliyopo, Dira ya Taifa ya 2025.

Vile vile walikubaliana kuendeleza mjadala kuhusu kuzingatia usawa wa jinsia 50/50 katika yanja zote za uongozi. Mwisho wanamtandao walikubaliana kuendeleza jitihada za kuimarisha tapo ili kuendeleza madai ya haki za wanawake na wasichana kwa jumla.




**Picha**: Moja ya kongamano liliondaliwa na Mtandao kutafakari namna ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika michakato ya demokrasia

## 2.1 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA MTANDAO TANGU 2014 HADI 2024

Kwa kutambua kwamba kazi ya kushinikiza mabadiliko ya mfumo mpana wenye kubagua na kukandamiza wanawake na wasichana ni kubwa, wanamtandao walikubaliana kwamba kuundwe kamati ya ufundi (technical Committee) yenye uwakilishi wa asasi 15 ambayo itashughulika kubuni mikakati mpya na endelevu ya kuimarisha Tapo na kuendeleza ujenzi wa ajenda moja na sauti moja kwenye kudai haki za msingi za wanawake na wasichana. Vile vile Mtandao ukapendekeza mgawanyo wa majukumu yakizingatia maeneo nyeti yanayoshughulikiwa na mtandao.

Kubuni mikakati mipya na endelevu ya kuimarisha Tapo

Kupendekeza mgawanyo wa majukumu yakizingatia maeneo nyeti yanayoshughulikiwa na mtandao

**15** Asasi zinazounda Kamati ya kitaalam

Kuendeleza ujenzi wa ajenda moja

Kuendeleza sauti moja kwenye kudai haki za msingi za wanawake na wasichana




**Picha**: Moja ya mikutano ya kamati kujadili mikakati ya kuimarisha mtandao

## 2.2 MGAWANYO WA KAZI KIMASHIRIKA ULIKUWA KAMA IFUATAVYO

### A. KURATIBU SHUGHULI ZOTE ZA MTANDAO:

Kazi hii ilikabidhiwa kwa WFT ikisaidiwa na Kamati ya Kitaalam (Technical Committee) inayoundwa na mashirika wanachama 15. Shughuli za kiuratibu, ambazo ziliendelezwa chini ya program au dawati la Ushinikizaji ndani WFT, ni pamoja na kuaandaa mpango kazi wa Mtandao, kutoa mwelekeo wa Kifikra (conceptual leadership) kwa kuwajengea wanamtandao uelewa wa pamoja.

### B. KUTANDAA NA KUFIKIA JAMII (COMMUNITY OUTREACH):

Kazi hii ilikabidhiwa kwa TGNP ikishirikiana na wanachama wengine wa Mtandao ili kupanua wigo wa Mtandao ili kufikia jamii nyingi zaidi na kuwawezesha wanawake katika ngazi ya jamii kupaaza sauti zao ili kuongeza nguvu ya pamoja katika kudai haki zao za kikatiba.

### C. KUTUMIA VYOMBO VYA HABARI:

Kazi hii ilikabidhiwa kwa TAMWA ili kuwaongoza wanachama wengine wa Mtandao kuhusu jinsi ya kutumia vyombo vya habari katika mchakato wa kushinikiza Katiba Mpya ibebe msingi wa usawa wa kijinsia; kuandaa mpango kazi na kuratibu uandishi wa makala mbalimbali na utoaji wake kwenye vyombo vya habari

### C. KUVUNJA MIPAKA YA KITIKADI ZA KISIASA:

Kazi hii ilikabidhiwa kwa ULINGO ambayo ilipewa jukumu la kuunganisha nguvu kati ya Wanamtandao na wanawake na kuhamasisha wanawake kutoka vyama vya siasa mbalimbali kuvunja mipaka ya kiitikadi na kuunganisha nguvu zao katika kudai haki za wanawake za kikatiba, hususani kuwezesha kubomoa mifumo inayowabagua wanawake katika meza za maamuzi.

### D. KUBAINISHA MASUALA YA KISHERIA YANAYOHALALISHA UBAGUZI WA JINSIA:

Jukumu hili lilikabidhwa kwa TAWLA ambayo iliwaongoza Wanamtandao katika kufuatilia masuala ya kisheria kwenye kuainisha mapengo yaliyopo katika sheria zetu ikiwa ni pamoja na vipengele vianavyokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### E. KUFIKIA WANAWAKE WENYE ULEMAVU:

Jukumu hili lilikabidhiwa kwa shirika la SWAUTA na linajumuisha uhamasishaji wa wanawake wenye ulemavu nchini kuungana na Mtandao ili madai yao mahsusi ya kikatiba yaunganishwe kwenye madai mengine yanayoshinikizwa na Mtandao wa Wanawake na Katiba Tanzania.

## 2.3 KUIMARISHA/UJENZI WA TAPO LA UTETEZI WA HAKI ZA WANAWAKE

Wanamtandao walitambua kwamba, kwenye muktadha unaoongozwa na soko huria katika Nyanja za uchumi, kuna uhitaji wa kujenga nguvu za pamoja kwanza za kukabiliana na mfumo mpana unaoashiria kuacha sehemu kubwa wa watu duniani katika umaskini na ufukara, ambao wanawake wanabeba athari zake zaidi. Ili kuimarisha Tapo juhudi za makusudi zilitumika ili kujenga uelewa wa pamoja wa ajenda tunayoipigania.

Tafakari za kina kuhusu dira na maono ya Wanamtandao Wanamtadao walianza kutafakari kwa kina muktadha wetu kwa wakati ule, wakijihoji:

01 Ni kitu gani kinachotutambulisha kama wanawake licha ya tofauti zetu katika maeneo mengi ya kiuchumi, kiimani na hata kiitikadi?

02 Ushiriki wetu katika siasa unongozwa na dira ipi na ajenda zipi?

03 Kujengeana uwezo ili kuwa na uelewa wa mukadha, fursa zilizozoko na changamoto zake. Mbinu zilizotumika ni pamoja na mafunzo, mijadala ya rika, kongamano na mikutano, pamoja na utafutaji wa rasilimali kwa kutumia fursa iliyojitokeza kwa kuwepo kwa Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania




**Picha**: Washiriki wa Kongamano la Kitaifa la Wanawake wakifuatilia mada kuhusu safari ya Mtandao huo

## 2.4 UCHAMBUZI WA SHERIA ZA UCHAGUZI

Wanamtandao wa Wanawake Katiba, Uongozi na Uchaguzi walitambua kwamba, lazima kuweko na mifumo ya sheria, sera na mipango ya kujenga utamaduni wa siasa uliojikita katika msingi inayoongozwa na usawa na haki za wanawake na wanaume. Kutokana na uelewa huu wa pamoja, Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi uliona umuhimu wakuchambua baadhi ya sheria kandamizi kwa lengo la kushinikiza mabadiliko na maboreshe kwa kuzingatia mrengo wa jinsia. Suala la sheria lilipewa kipaumbele.

Chambuzi za sheria za uchaguzi ziliongozwa na misingi hii

01 Ushindani ulio huru na haki kwa mrengo wa jinsia(Fair competition)

02 Usawa wa jinsia katika Nyanja za maamuzi

03 Uwazi katika maamuzi ya uteuzi ndani ya vyama na katika matumizi ya rasilimali za vyama kwa kuzingatia usawa wa jinsia

04 Utawala wa sheria kwa mrengo wa jinsia

Misingi hii ilipelekea Mtandato wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi kuanza na mchakato wa kufanya uchambuzi yakinifu wa sheria, miongozo na sera zinazoongoza au kuwezesha au kukwamishwa kwa ushiriki wa wanawake katika meza za maamuzi.

Sheria zilizoainishwa na Mtandao za awali ni:

- Pamoja na sheria za Uchaguzi ikiwa ni pamoja na Sheria ya Uchaguzi (CAP 343) (R.E. 2015)
- Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar (20150
- Sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa na Mamlaka za Miji (CAP 288(R.E.2002)
- Sheria za Vyama vya Siasa CAP 258)
- Sheria ya Gharama za Uchaguzi (CAP 278(R.E 2015)
- Sheria ya Tume ya Uchaguzi

Licha ya hizi sheria za uchaguzi, uchambuzi yakinifu ulifanywa kwenye taratibu, miongozo inayosimamia uchaguzi kwa njia moja au nyingine. Miongozo inayoongoza utendaji wa vyombo vingine wakati wa uchaguzi. Vile vile Wanamtandao walifanya uchambuzi yakinifu wa Muswada wa Uchaguzi wa mwake 2023.







**Picha**: Baadhi ya wanamtandao wakizungumza na wanahabari kuhusu mapendekezo ya mtandao kwenye sheria za uchaguzi

### 2.4.1 Madai ya wanawake kuhusu Maboresho/mabadiliko Ya Sheria za Uchaguzi na Vyama vya siasa.

**01** Sheria zibainishe na kulinda haki ya wanawake katika ushiriki katika uchaguzi kwa kuzingati msingi wa kufikia 50/50 katika meza za maamzi

**02** Kwamba , Sheria zielekeze mabadiliko kwenye Mfumo wa Viti maalum vya wabunge na madiwani ili kuwezesha wanawake kuchaguliwa na wapiga kura kama wanaume. Kwenye hili, sheria ibainishe mfumo utakaowezesha kila jimbo kuwa na wagombea wawili ktuka vyama na hatimaye kuwa na wawakilishi wawili kwenye majimbo ya uchaguzi

**03** Sheria zielekeze vyombo vya habari hususani vinavyomilikiwa na umma kutoa fursa sawa kwa wanawake wakati wa kampeni

**04** Sheria ziongezee makosa ya ukatili na unyanyasikaji wa jinsia wakati wa uchaguzi kwenye orodha ya makosa na adhabu yanayotokana na uchaguzi

**05** Sheria zitumie lugha jumuishi

**06** Sheria iwajibishe vyama vya siasa kuzingatia misingi ya usawa wa jinsia katika ushiriki wa wanawake katika uongozi wa vyama, katika uteuzi wa wanaowania nafasi katika chaguzi, na ketenga rasilimali ya kuwawezesha wanawake kushinda

**07** Kwamba, Sheria ya vyama ibainishe misingi ya uwajibikaji wa uongozi wa vyama kwa wanachama wao husuan kwa wanawake hasa kwenye kuwalinda dhidi ya ukatilai wa jinsia wakati wa chaguzi

**08** Kwamba, sheria ilekeze Matumizi ya rasilimali fedha wakati wa uchaguzi uzingatia mahitaji maalum kwa wanawake wenye kuwania nafasi za uongozi ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za uchaguzi.

**09** Kwamba, sheria zizingatie matumizi ya lugha jumuishi kwa mrengo wa jinsia

### 2.4.2 Mapengo Yaliyoibuliwa katika Chambuzi za Sheria za Uchaguzi na sheria ya vyama vya siasa

Mfumo wa uchaguzi unaotumika katika mchakato wote wa uchaguzi siyo wezeshi kwa ushiriki wa wanawake.

1. Kwamba mfumo wa ushindani hauko huru wala wa haki kwa wanawake wenye kuonesha nia ya kushiriki
2. Mfumo wa kuongeza wanawake kwa kupitia viti maalum umehalalisha ubaguzi na kujenga tabaka la stahiki na haki tofauti kati ya wanawake wanaochaguliwa kwenye majimbo na hawa wa viti maalum. Kwamba wa viti maalum hawastahli mfuko wa jimbo wala kustahli nafasi mbalimbali za uteuzi kama vile ya Waziri Mkuu.
3. Kwamba hakuna njia wazi na huru ya uteuzi wa wanawake wanaowamia kushiriki ndani ya vyama. Kwamba sheria za uchaguzi haziwajibishi vyama vya siasa kuzingati misingi ya uswa iliyobainishwa kwenye mikataba ya kimataifa, kikanda na hata kwenye katiba.
4. Rasilimali za vyama hazitumiki kwa njia ya uwazi na pia hakuna mikakati ya kushughulikia vikwazo vinavyowakumba wanawake wanapooneshakuwania nafasi.
5. Mara nyingi wanawake wanaotia nia ya kugombea hukabiliwa na ukatili wa jinsia ikiwa ni pamoja na matusi, na madai ya rushwa ya ngono.
6. Lugha zinazotumika kwenye sheria siyo jumuishi.

### 2.4.3 Matokeo:

Uchambuzi wa mabadiliko ya sheria za uchaguzi pamoja na  Sheria Mpya ya Uchaguzi ya mwaka 2003 ulibaini kwamba, misingi ya usawa wa jinsia hususan dai la 50/50 halikukubalika, na masuala ya jinsia kwa jumla hayakuzingatiwa ikiwa ni pamoja na uteuzi wa Rais na Makamu wake, uteuzi wa Wabunge, kuendeleza kuwepo kwa mfumo wa viti Maalum, gharama za uchaguzi na athari zake kwa wanawake wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali.

Vile vile , makosa na adhabu kwenye mchakato wote wa uchaguzi zitokanazo na masuala ya ukatili na ubaguzi wa jinsia hayakubainishwa kwenye orodha ya makosa na adhabu katika mchakato wa uchaguzi.Kwa ufupi madai ya wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi hayakuzingatiwa katika sheria mpya za uchaguzi. Sheria zisipozingatia masuala ya uchaguzi, miongozo na maelekezo yatakayotokana na sheria husika hazitaongozwa na misingi ya usawa wa jinsia. HIvyo basi, wanawake wataendelea kushiriki katika mchakato wa uchaguzi katika uwanja ambao siyo sawia.

### 2.4.4 Mafanikio

Mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa , yaliingiza msingi wa usawa wa jinsia kama ulivyokuwa umeainishwa kwenye mabadiliko ya sheria ya mwaka 2019 kifungu cha 6A(2) ambacho kilivitaka vyama vya siasa viongozwe na misingi ya kikatiba ya demokrasia, utawala bora na isiyobagua).

Sisi wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi tunakiri kwamba hili ni fanikio kubwa. Vile vile Sehemu ya Tatu  Kifungu cha 9 kimerekebishwa kwa kuingiza Kifungu kipya 10C kinachowajibisha vyama vya siasa kuwa na nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na sera ya jinsia na jumuishi ya makundi maalum. Kifungu hiki cha 10C kimebainisha mambo yatakayohitajika kuweko kwenye Sera ya Jinsia na Jumuishi  ikiwa ni pamoja na:

01 Kuweko kwa program zinazoonesha kuwezesha utekelezwaji wa sera hii

02 Kuwepo na program ya kujenga uwezo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

03 Kuweko kwa dawati la jinsia la kusimamia na kuratibu utekelezwaji wa sera hii ya jinsia,sheria, sera,na kushughulikia manung'uniko kuhusu masuala ya jinsia

Kwetu sisi wanamtandao, tulikiri kwamba vipengele husika ni  fanikio endapo vifungu hivi vitapewa miongozo ya utekelezwaji katika shughuli zote za vyama ikiwa ni pamoja na matumizi ya rasilimali watu na fedha za vyama kuwezesha kuendesha sera ya jinsia katika mipango ya kuondoa pengo la jinsia, kuendesha shughuli za dawati la jinsia na katika kuwajengea wanawake uwezo wa ushiriki katika mchakato wote wa uchaguzi.

**01**

"kwenye mabadiliko ya sheria ya mwaka 2019 kifungu cha 6A(2) ambacho kilivitaka vyama vya siasa viongozwe na misingi ya kikatiba ya demokrasia, utawala bora na isiyobagua)."

**02**

"Sehemu ya Tatu Kifungu cha 9 kimerekebishwa kwa kuingiza Kifungu kipya 10C kinachowajibisha vyama vya siasa kuwa na nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na sera ya jinsia na jumuishi ya makundi maalum."



**Picha**: Aliyekua Mwenyekiti wa Mtandao Prof. Ruth Meena akikabidhi mapendekezo ya mtandao kwa Msajili wa vyama vya siasa

# 2.5 KUSHINIKIZA KUSITISHWA KWA MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA SHERIA YA KUPAMBANA NA RUSHWA YA NGONO

Tanzania ni kati ya nchi chache Barani mwa Afrika iliyoweza kuingiza Rushwa ya Ngono kwenye sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007. Kifungu cha 25 kuhusu rushwa ya ngono, kilitokana na chachu ya Chama cha Wanawake Majaji nchini, ambao kutokana na uzoefu wao wa sheria na makosa yanayoendana na ngono, waliwezesha kuongoza serikali yetu kuingiza kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa hapa nchini.

Majaji hawa wanawake walitofautisha rushwa za kawaida na rushwa ya ngono kwa maana rushwa ya ngono inatokana na tafsiri tofauti katika dhana nzima ya mahusiano ya kimamlaka. Vile vile walitofautisha biashara ya ngono na rushwa ya Ngono kwa maana kwenye biashara ya ngono watu wawili wanakubaliana kubadilishana ngono kwa vitu yakinifu. Kimantiki, rushwa ya ngono inatokana na mahusiano ya kimamlaka pale ambapo mwenye mamlaka anadai ngono kwa sharti la kutoa stahiki au upendeleo.

Kwa kuzingatia kanuni na miiko ya uongozi ziilizobainishwa katika miongozo mbalimbali yenye kukataza wenye mamlaka kuwa na mahusiano ya kingono na wale wanaowaongoza, kifungu 2 5 cha sheria hii kililenga kuwawajibisha wenye mamlaka kufuata miiko ya uongozi katika nyadhifa walizopewa dhamana ya kuzisimamia. Kifungu hiki katika sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini, kiliipa Tanzania hadhi kubwa kimataifa kwenye eneo la utetezi wa haki za wanawake, wasichana na watoto wa kike na wakiume.

Baada ya kuielewa sheria hii, watetezi wa haki za wanawake na watoto waliunganisha nguvu zao na kuunda Mtandao Dhidi ya Rushwa ya Ngono mwaka 2000. Mtandao huu unaojulikana kama "Mtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania" unaounganisha takribani asasi za kiraia zaidi ya mia mbili (200), ulianza shughuli zake rasmi tangu mwaka 2013, ukiwa na lengo kuu la kuunganisha nguvu za pamoja za kupinga vitendo vya rushwa ya ngono nchini.

Mtandao dhidi ya rushwa ya ngono ulianza kampeni yenye lengo la kuelimisha umma wa Tanzania kuhusu dhana nzima ya rushwa ya ngono ikiwa na kauli mbiu "Vunja Ukimya Rushwa ya Ngono Inadhalilisha na Inaua" Wanamtandao huu wanaamini kwamba, Rushwa ya Ngono ni tishio kubwa la kijinsia kwa wahanga na inadhalilisha utu na heshima ya Taifa letu. Vile vile wanamtandao huu wanaamini kwamba rushwa ya Ngono inakiuka misingi yote ya haki za binadamu husasan za wanawake na watoto kama zilivyobainishwa katika mikataba, makubaliano, maagano, na maagizo mbalimbali ya Kimataifa Kikanda na hata kwenye Katiba ya nchi yetu,[2].






**Picha**: Moja ya mikutano na wanahabari kuhusu Rushwa ya Ngono

[2] Mikataba hii ikiwa inajumuisha Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Tamko la Beijing 1995 na Mpango Kazi wa Beijing mwaka 1995, Mkataba wa Haki za Watoto (CRC), na The Solemn Declaration of AU, na pia Makubaliano mbalimbali ya Kutetea Haki za Wanawake SADC

Kwa kiwango kikubwa mtandao huu wa kupinga rushwa ya ngono umefanikiwa kuhamasisha jamii kuelewa kwa kina suala zima la ukatili wa kingono na hasa rushwa ya ngono. Kampeni ya "kuvunja ukimya" kuhusu rushwa ya ngono imefungua fursa kwa wananchi na haswa kwa wahanga wa unyanyasaji huu na hivyo kuonezeka katika kujitokeza na kutoa shuhuda nyingi zilizoonesha ukubwa wa tatizo la rushwa ya ngono kwenye kila sektra ya jamii yetu nchini. Baadhi ya shuhuda hizo ni pamoja na:

01 Wafanya kazi wa majumbani walioweza kupaza sauti kuhusu kudaiwa rushwa ya ngono na waariji wao kama sharti la kuongezewa mishahara, kupewa likizo au kutokafukuzwa kazi. Pale mfanya kazi alipodiriki kukataa, aliachishwa kazi na mara nyingi bila kulipwa mishahara yake.

02 Wafanyakazi katika taasisi za umma, wanawake kwa wanaume, wamekiri kulazimishwa kutoa rushwa ya ngono ili wapandishwe vyeo, waongezewe mishahara au wapewe stahiki nyinginezo za kikazi. Wale waliodiriki kukataa mashariti hayo waliachishwa kazi, kunyimwa vyeo au kuchukuliwa hatua za kinidhamu pasipo uthibitisho wa kuonesha uvunjwaji wa nidhamu kazini. [3]

03 Kwenye elimu, zipo sauti za watoto wa shule wa kike na kiume waliokiri kulazimishwa kutoa ngono na waalimu wao, ili wafaulishwe au kupewa upendeleo kwenye shughuli za shule.

04 Wanafunzi wa vyuo vikuu nao walipaaza sauti zao wakidai kulazimishwa kutoa rushwa ya ngono na wahadhiri, wakufunzi na hata maprofesa wao ili wapewe alama za juu kwenye mitihani au kazi zao za masomo. Kwa wale ambao walikataa wengi wao wamefelishwa, wengi kukata tamaa na kusitisha masomo yao na wachache wao iliwagharimu maisha kwa kujiua.

05 Kwenye watoa huduma za afya, wapo kina mama waliopaaza sauti zao kuhusu kudaiwa ngono ili aidha watoto wao wahudumiwe au wao wenyewe wahudumiwe wakati walipohitaji huduma za uzazi na nyinginezo.

06 Pia wenye vyombo vya usafirishaji hususan boda boda na dala dala wamekiri kudai rushwa ya ngono kwa watoto wasiyoweza kulipia nauli ili wawape usafiri bure. Baada ya kuhamasisha kundi hili, vijana wengi wa bodaboda na madereva wa dala dala kwenye mji kama Dar es Salaam, wamekuwa mabalozi kwenye kuwalinda watoto wa shule dhidi ya vitendo hivi kwenye vyombo vya usafirishaji.




[3] Tuna shuhuda ya mwanamke mmoja aliyipambana kudai haki ya kurejeshwa kazini kwa takribani miaka nane, kwa kudirikikumkatalia kiongozi wake vishawishi vya rushwa ya ngono. Katika kipindi hiki kila alipodai haki kuna waliotaka awape rushwa ya ngono, hivyo ikachaukua miaka mingi kudai haki zake akiishi maisha magumu bila mshara, na mara nyingine akiwa ombaomba kwa ajili ya fedha za kujikimu. Hata mahakama ilipoamuru arejeshwa kazini, ilimchukua mwaka mmoja kwa amri ya mahakama kutekeleza na mwajiri wake.

Pamoja na jitihada za kuhamasisha jamii kuelewa na kukataa na kupinga rushwa ya ngono, TAKUKURU ilipendekeza mabadiliko ya sheria hii kwa kuongeza kifungu kidogo 25(2) kinachosomeka,

> Mtu yoyote, ambaye, amemsababishia mwenye mamlaka, kufanya kosa hili kwa kumwahidi, kumshawishi, kwa kutoa rushwa ya ngono ili apendelewe, apewe cheo, ajira, au kupandishwa cheo anakuwa hatiani kwa kosa la rushwa ya ngono na kustahili adhabu ya fedha za Kitanzania zisizopungua million mbili au kuzidi million kumi au kifungo cha jela kwa miaka isiyopungua mitano au kuzidi miaka kumi
>
> **- (Tafsiri)**

Kwa maoni ya wanamtandao, kifungu hiki cha nyongeza kinapokonya (clawback) haki na ulinzi ulioko kwenye kifungu mama cha 25. Kwa hivyo Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Nchini walikataa kifungu hiki kidogo, 25 (2) na kunadai kiondolewe kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria hii.

Wakiunganisha nguvu na mitandao yote inayotetea haki za wanawake na wasichana, kwa sauti moja na kauli moja, Wanamtandao na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi ya kutetea haki za binadamu kwenye mazingira ya uonevu, wakiwemo hasa wanawake, wasichana, wanaume na vijana wa kiume wasio na sauti, walisema " hatukubaliani na marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu 25 kilicho ongezewa kifungu 25 (2) kama ilivyojitokeza hapo juu. Kifungu hiki ni cha uonevu na upotoshwaji wa haki kwa kuwa kina lengo la kutaka mhanga wa rushwa ya ngono ashitakiwe endapo itathibitika kwamba, yeye "alimsababisha mwenye mamlaka kufanya kosa" hili kwa "kumshawishi au kumwahidi" ngono ili apewe haki au apendelewe.

> "Hatukubaliani na marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu 25 kilicho ongezewa kifungu 25 (2) kama ilivyojitokeza hapo juu. Kifungu hiki ni cha uonevu na upotoshwaji wa haki kwa kuwa kina lengo la kutaka mhanga wa rushwa ya ngono ashitakiwe endapo itathibitika kwamba, yeye "alimsababisha mwenye mamlaka kufanya kosa" hili kwa "kumshawishi au kumwahidi"

Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Nchini

Vile vile Wanamtandao na washiriki wengine wapenda maendeleo na haki, ha wakukubaliana kabisa na sababu zilizotolewa na Takukuru kuhusu marekebisho haya kwa upande wa rushwa ya ngono. Sababu hizo ni pamoja na kwamba:

01 Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa jumla imepitwa na wakati

02 Sheria hiyo haijazingatia makubaliano ya kimataifa kuhusu Rushwa (ikiwemo rushwa ya ngono)

03 Kuwepo kwa mabadiliko ya TEHAMA yanayohusisha miamala ya ki elektroniki ambayo hayakuwepo ama yalikuwa kwa uchache, video nukushi wakati sheria hii ilipotungwa miaka kumi iliyopita

04 Kuwepo kwa mabadiliko ya mitindo ya maisha ambayo yameleta na kuibua changamoto zaidi ambapo vitendo vya rushwa ya ngono vimefika mpaka kwa wanafunzi wa shule

Wanamtandao na watetezi wa haki za wanawake na watoto hapa nchini, walikiri kwamba, sababu hizi hazina mshiko kwenye suala la rushwa ya ngono, na hazitokani na hali halisi ya rushwa ya ngono na athari zake kwa wananchi na haswa wahanga nchini, bali zinaendeleza kuwalinda wenye mamlaka (na wanaoendelea kutumia madaraka hayo vibaya) katika kuendelea na vitendo hivi ambavyo vinaathiri mhanga na kumpokonya utu wake, na kwa wengine imesababisha vifo na kuathiri kwa kiwango kikubwa utu wa taifa letu na uchumi wetu.

Ni ukweli usiopingika kwamba, mabadiliko ya mtindo wa maisha nchini na kwingineko kumezalisha changamoto kubwa hususani kuhusu ukatili wa jinsia dhidi ya wanawake, wasichana na hata vijana wa kiume. Kutokana na hili, nchi yetu sharti iweke na kubuni mikakati mbadala ya kulinda na kutetea wanawake na makundi yote yanayodhalilishwa, kwani mabadiliko hayo yamewasababishiawanawake majeraha ya ziada na kuongeza ukatili dhidi yao. Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono kilihitaji uimarishwaji kwenye kutekeleza na siyo kuongeza kifungu kinachopokonya haki iliyobainishwa katika kifungu cha sheria hii (claw back clause).

Vile vile Wanamtandao walihamasisha jamii ya Watanzania wote, wanawake kwa wanaume, wakatae mapendekezo ya mabadiliko haya ya sheria hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Ya Ngono (2022/23): Kifungu 25/2, hayatokani na tafiti na shughuli nyingi ambazo Wanamtandao na makundi mbalimbli ya kijamii walizokuwa wakifanya kwa kushirikiana na TAKUKURU kwenye eneo hili ikiwa ni pamoja na tafiti, kuendesha elimu na kampeni kubwa ya kupinga vitendo vya rushwa ya ngono wakiongozwa na kautli mbiu "Vunja Ukimia, Rushwa Ya Ngono Inaua na Kudhalilisha"

> "Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono kilihitaji uimarishwaji kwenye kutekeleza na siyo kuongeza kifungu kinachopokonya haki iliyobainishwa katika kifungu cha sheria hii (claw back clause)."

Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Nchini

Kwa mfano, katika uzinduzi wa kampeni ya Kupambana na Rushwa ya Ngono huko Shinyanga iliyozinduliwa tarehe 17 Desemba 2022, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga (ACP Janeth Magomi alinukuliwa akisema;

"Rushwa ya Ngono inaanzia nyumbani na kazini ambapo watu wenye mamlaka wanatumia mamlaka yao vibaya wakitaka wapewe rushwa ya ngono ambapo rushwa hii inamuumiza zaidi mwanamke. Huko mtandaoni pia wanawake wanaombwa rushwa ya ngono pale wanapotishiwa picha zao kusambazwa mtandaoni. Rushwa ya ngono inasababisha tupate wataalamu wasio na sifa lakini pia inaua kutokana na kuchangia maambukizi ya magonjwa ya zinaa ukiwemo UKIMWI, na inamfanya muathirika wa rushwa ya ngono kuwa mtumwa wa ngono Rushwa ya ngono ni unyanyasaji, kunyamazia kimya rushwa ya ngono ni kunyima haki. Kila mtu aguswe na athari za rushwa, kila mmoja apaze sauti. Naomba wananchi mtoea taarifa polisi na TAKUKURU kuhusu vitendo vya rushwa ya ngono na rushwa zingine. Tukipata taarifa hizo tutazishughulikia kwa weledi na usiri mkubwa".

**ACP JANETH MAGOMI**
Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga

Matokeo ya Tafiti zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na TAKUKURU pamoja na shuhuda zitokanazo na elimu ya kuhamasisha umma kuilewa Sheria ya Kupambana, ikiwemo kupambana na rushwa ya ngono kwenye taasisi za umma, zikiwemo za taasisi za Elimu ya Juu, zinonesha kuwepo kwa tatizo hili, likiwa limesababishwa na matumizi mabaya ya wenye mamlaka, udhaifu kwenye mifumo ya kuwajibisha wenye mamlaka, na tabia za kulinda wenye mamlaka.

Mambo haya yanachangia kupunguza uwajibikaji na hatimae kuongezeka vitendo vya rushwa ya ngono katika taasisi za umma, na za binafsi, kwa watoa huduma kama vile sekta ya afya, mahakama, na hata ndani ya majumbani mwetu.

Aidha, imebainika wanaoshiriki vitendo vya rushwa, ikiwemo rushwa ya ngono ni watu wenye mamlaka katika ngazi zote za uongozi ndani ya taifa letu. Hivyo basi, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007, kifungu cha 25 cha sheria hii kina haramisha kitendo chochote cha mtu mwenye mamlaka kumuwekea kigezo cha ngono mtu yeyote anayetaka huduma kutokana na ukiukwaji huu uliobainika, kuna umuhimu wa kuweka mikakati ya kuimarisha mifumo ya udhibiti wa vitendo hivi.

Vile vile, athari zinazotokana na tatizo hili, ni pamoja na kuzima ndoto za wahanga, hususani wanawake, na wasichana, na kusababisha wahanga wa janga hili kuwa watumwa wa ngono na vifo kutokana na kushindwa kumudu jeraha za rushwa ya ngono, pamoja na athari pana kwenye utu wa taifa letu na uchumi wake.

### 2.5.1 Mapendekezo ya Mtandao

Kwa kuzingatia kwamba, kampeni hii ya kitaifa imeshafikishwa mbali na wadau wengi, hasa wa ngazi za jamii hapa nchini, ambapo wanajamii hawa wakishirikiana na wale wa ngazi za kitaifa walishaibeba na kwa upande mkubwa kuleta mabadiliko ya kifikira na hata kitabia, kutokana na shahidi, zakitakwimu zinazoonesha kuwa wengi wa waathirika wa matukio ya rushwa ya ngono walishaanza kuvunja ukimya wa uonevu huu na kutaja wahusika.. Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania na washiriki wote wanaopigania haki za binadamu na makundi ya wanyonge, walipendekeza yafuatayo kuhusiana na maudhui yahusuyo rushwa ya ngono katika Sheria ya Marekebisho ya Kuzuia na Kupinga Rushwa (2023)Walipendekeza kwamba:

**01** Mchakato uliokuwa unaendelea na maandalizi ya kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kupinga Rushwa usitishwe na Waziri mwenye dhamana, asipitishe marekebisho yanayopendekezwa na TAKUKURU kwa vile maoni ya wadau wengi hayakuzingatiwa kwenye mchakato huu. Hata hivyo wanamtandao walisisitiza kwamba:

**A.** Endapo Wizara yenye dhamana itapitisha mapendekezo haya, na kupeleka bungeni bila ya marekebisho yanayohitajika, tunawashauri Wabunge wetu (kwa ujumla wao) wasipitishe sheria hii, kwani sisi kama sehemu kubwa ya wapiga kura wao tunaikataa kwa kauli moja.

**B.** Na, endapo Bunge letu tukufu litaamua kuipitisha sheria hii, basi tunasihi na kumshauri Raisi wetu, mtetea haki za wananchi, wakiwemo wanawake na waasichana, asikubali Sheria hii kwa kuwa utekelezaji wake, utakuwa wa kibaguzi na udhalilishaji wa wale wasio na madaraka nchini.

**02** Marekebisho yanayopendekezwa kwenye Sheria hii yaKuzuia na Kupambana na Rushwaibaki na kifungu cha 25 cha mwanzo kama kilivyosimama, na kifungu cha 25(2) kisiwepo na kifutwe kwani kifungu hicho hakiongezi tija yeyote zaidi ya kuijengea sheria hii mazingira ya kuendeleza mifumo dume kandamizi na matumizi mabaya ya waliokabidhiwa mamalaka katika mikutadhi mbalimbali nchini.

**03** Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono nchini walihoji dhamira ya mapendekezo ya hiki kifungu cha 25(2) wakati huu tunapoongozwa na Rais Mwanamke mtetezi wa haki za wote na hasa za wanawake, watoto na makundi yolioko pembezoni.

Tunajiuliza, ni kwanini sasa? Sheria hii ilitungwa wakati wa uongozi wa awamu ya nne, ikaanza kutekelezwa kwa vishindo awamu ya tano wakati asasi za kiraia zilipoungana na taasisi za umma kuelimisha, kutafiti na kuwezesha wananchi na haswa wahanga kukataa rushwa ya ngono bila woga au kuficha. Katika hali hii, tunahisi mbinu za kuhujumu hatua zinazochukuliwa na Mh. Rais katika utetezi wa haki za wanawake na makundi yaliyoko pembezoni nchini.

**04** Wanamtandao wanaopinga Rushwa ya Ngono, tunatoa wito kwa wale wote wanaohusika na maandalizi ya sheria hii, ikiwa ni pamoja na TAKUKURU, wizara yenye dhamana ya kuaandaa sheria, kutusikiliza sisi wadau wakiwemo wadau wanaofanya nao kazi kwa kupitia Mitandao mbalimbali ya kiraia na inayo tetea haki za wanawake, wasichana na makundi mengine ya wasio na sauti nchini.

05 Wanamtandao wanaopinga Rushwa ya Ngono, walitoa wito kwa wanamtandaowote watetezi wa haki za wanawake na washichana wanaendelea kupinga mabadiliko haya wasipotoshe umma kwa kuchanganya dhana ya rushwa ya ngono na biashara ya ngono na hivyo kuitumia mantiki ya 'mtoa rushwa na mpokea rushwa, mshawishi na anaye shawishika' (Demand and Supply).

Walitoa n rai kwa umma wa Tanzania kuelewa na kutofautisha dhana hizi mbili, kwa kuwa biashara ya ngono inatasifiriwa kuhusiana na watu wawili waliokubaliana kubadilisha ngono kwa vitu yakinifu, (hapa kuna "makubaliano" kati ya anayetoa na anayepokea), wakati kwenye dhana ya rushwa ya ngono kama shuhuda zilivyoonesha, ni mtu mwenye mamlaka kutoa stahiki au upendeleo kwa sharti la ngono (power relationship), na suala la kutaka kuonyesha kuwa mhanga ana nguvu za kumshawishi mwenye mamlaka afanye tendo hilo, wakati hili si kweli bali ni uonevu.

06 Wanamtandao walitoa wito kwa Watanzania wote kutokukubalikuwalinda hawa wachache wenye mamlaka kuchafua heshima ya taifa letu na wanaoendeleza vitendo vya kunyanyasa na kuwapokonya haki wale tuliowapa dhamana ya kuwalinda, kuwatetea na kuwaongoza.

07 Vile vile walitoa wito kwa TAKUKURU (na washiriki wake) kuchukua hatua stahiki kusitisha mchakato wa kuingiza kifungu cha 2 kwenye sheria hii na kuelezea umma kwa uwazi athari za kuwepo kwa kifungu hiki kinachowapokonya wanachi na haswa wahanga wa rushwa ya ngono haki zao za msingi, na kurudisha taifa letu nyuma katika uteteze wa haki za binadamu hususan za wanawake, watoto na makundi yalioko pembezoni.

### 2.5.2 Mafanikio

Hatima ya mapendekezo haya hatujui kwani mapendekezo ya Takukuru bado yako kwenye meza ya Mwanasheria Mkuu. Tunataka kujiaminisha kwamba sauti zetu zimesikika na madai yetu yatazingatiwa katika kuboresha hii sheria.



## 2.6 SHERIA YA NDOA VIFUNGU VINAVYORUHUSU NDOA ZA UTOTONI

Sheria mbalimbali za Tanzania zinatoa tafsiri tofauti na zenye kukizanza kuhusu umri wa mtoto na hasa mtoto wa kike, pamoja na stahiki na haki tofauti. Kwa mfano, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sehemu ya Tatu kuhusu haki na Wajibu wa Usawa Kifungu cha 12.-(1) kinakiri kwamba Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa. Kifungu 12- (2) kinakiri, kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Ambapo kifungu 13.-(1) kinatamka kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.Kifungu 13- (2) kinapiga marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake (URT: 1977).

Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 Sura ya 29, 9(1) kinatafsiri ndoa kama ni muungano wa hiari kati ya mwanume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao. Hata hivyo kifungu cha 16 kinaelezea kwamba ili ndoa iwe ya kudumu lazima ijengeke kwenye misingi hii: (i) Hiari : kwa mantiki hii, udanganyifu, au ulaghai, kurubuniwa kwa aina yoyote unafanya muungano huo uiswe wa hiari. Hata hivyo sheria hii, kifungu cha 17 kinampokonya mwnamke haki ya kuwa huru na kuamua kwa hiari yake kuhusu ndoa .

Kifungu hiki kinaeleza kwamba mwanamke ambaye hajatimiza miaka 18 anaweza kuolewa akiwa na umri wa miaka 14 kwa ridhaa ya mahakama, au kwa miaka 15 kwaidhini ya baba, au kama baba amefariki mama na ikiwa wote wamefariki idhini hiyo inaweza kutolewa na mlezi. Hata hivyo umri wa vijana wa kiume wa kuoa ni miaka 18.

Vipengele hivi ni vya ubaguzi kwani vinatoa mwanya kwa watu wazima aidha kulazimisha, kushawishi au kumlaghai mtoto wa kike aolewe kinyume na utayari wake. Kwa tafsiri nyepesi Sheria ya ndoa inayoruhusu mtoto wa kike aolewe bila ridhaa yake.

Kwa kuzingatia misingi ya Kikatiba, Shirika la Utetezi wa haki za watoto na wasichana (Msichana Initiative) lilifungua kesi Mahaka Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupinga vipengele vilivyoko kwenye sheria ya ndoa kuhusu umri wa kuolewa kwa mtoto wa kike.

Baada ya ushindi wa kesi ya kihistoria katika Mahakama Kuu ya Tanzania iliyopelekwa na Rebecca Gyumi Mkurugenzi wa Mishana Initiative Mwaka 2016, akiomba mahakama ibatilishe vipengele vya sheria ya ndoa inayoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na Umri Mdogo kinyume na misingi ya katiba, Mwanasheria Mkuu alipinga uamuzi huu kwa madai kwamba dai hili linakinzana na tamaduni nyingi za jamii za Kitanzania.

Hata hivyo, Mahakama ya rufaa ya Tanzania ilitupilia mbali pingamizi ya Mwanasheria Mkuu, Kwa dai kwamba vifungu hivi vya sheria vinavyombagua mtoto wa kike katika suala la umri wa ndoa vinakinzana na haki za mtoto wa kike za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakati tukijiandaa kusherekea mafanikio haya, wanamtandao walishangazwa na uamuzi wa Bunge la Yamhuri Ya Muungano ya Tanzania lilipoamua kurudisha suala hili kwa jamii kujadili upya na kutoa maamuzi. Wanamtandao tutaendelea kushinikiza wabunge wetu waridhie maamuzi ya Mahakama ya Rufaa kwenye maamuzi yanayohusu haki za mtoto wa kike hasa kwenye suala la ndoa za utoto.

## 2.7 SHERIA YA AJIRA NA MAHUSIANO KUHUSU LIKIZO YA UZAZI KWA WANAWAKE WENYE KUJIFUNGUA WATOTO NJITI

Taasisi ya Doris Mollel ikiunganisha nguvu na mtandao wa utetezi wa haki ya afya ya Uzazi na asasi nyingine zenye kutetea haki za wanawake kwa jumla wamekuwa wakiendesha kampeni ya kudai maboresho ya sheria ya Ajira na Mahusiano ili kuongeza likizo ya uzazi kama sehemu ya kudai haki ya mtoto njiti kulelewa na haki ya mama aliyejifungua mtoto njiti kupata fursa wa kumtunza mtoto na kutunza afya yake.

Kampeni hii ilizaa matunda pale ambapo Makamu wa Rais kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania alitangaza kwa wafanyakazi wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu (2024) kwamba, kwa wanawake wafanyakazi katika sekta ya umm, likizo yao ya uzazi wanapojifungua Watoto njiti haitaanza wakati wa maangalizi maalum hadi hapo wataalamu wa afya watakapothibitisha kwamba mtoto amepita kile kipindi cha maangalizi maalum. Na kwamba wanawake hawa wataruhusiwa kufanya kazi hadi saa saba kwa kipindi cha miezi sita kuhakikisha kwamba Watoto hawa wanavuka kile kipindi hatarishi cha afya zao.

Kwa upande wa sekta binafsi, Makamu wa Raisi aliahidi kwamba serikali iko mbioni kurekebisha sheria ya Ajira na Mahusiano ili wanawake wote wenye kujifungua Watoto njiti wanuafaike na tamko hili. Kwetu sisi wanamtadao ni fanikio kubwa. Hata hivyo sisi wanamtandao tunaendelea kutetea kuendelea kudai nyongeza ya siku za likizo za uzazi kwa wanawake wote kwani siku 80 hazitoshi kumwacha mtoto ambaye ni nguvu kazi ya taifa hili chini ya uangalizi wa mtummwingine.




"Iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto njiti, kipindi cha uangalizi maalumu hakitahesabiwa kama likizo ya uzazi. Likizo ya uzazi itaanza baada tu ya kumalizika kwa kipindi hicho cha uangalizi,kadri madaktari watakavyothibitisha, Vile vile mfanyakazi husika ataruhusiwa kutoka kazini saa 7.30 mchana kila siku kwa muda wa miezi sita baada yakumalizika kwa likizo ya uzazi ili kumpa fursa ya Kwenda kunyonyesha,"

**- Mh. Dr. Philip Isdory Mpango**
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# 3.0 HITIMISHO

## TUKO WAPI? MAFANIKIO YAPI ? CHANGAMOTO ZIPI? NA MFUNZO YAPI

Masuala haya yataongelewa kwa kina zaidi kwenye tafakari za siku hizi mbili. Kwa ufupi, safari ya miaka zaidi ya mwongo mmoja ya Mtandao wa Wanawake Katiba, Uongozi na Uchaguzi , imefnikisha mambo mengi, tumepata changamoto nyingi, tumejifunza mambo mengi, na yote haya yanatupa mafunzo mengi ya kuongoza safari hii. Kwa kifupi

### 3.1 MAFANIKIO YA JUMLA NI KAMA YAFUATAYO:

01

Mageuzi kwenye Muktadha wa Kisiasa: Kwanza kabisa, kuwepo kwa Rais mwanamke kwa mara ya kwanza katika ke storia ya nchi yetu ni ni fanikio kubwa kwani linatupa fursa ya kuvunja imani potofu kuhusu nafasi ya mwanamke katika Nyanja za Uongozi katika ngazi hii ya juu iliyokuwa imehehodhiwa na wanaume kwa kipindi cha miongo sita.

Pamoja na kwamba Mh. Rais Samia Suluhu Hassan hakutokana na maboresho ya mifumo ya uchaguzi, kuwepo kwake kulikotokana na vipengele vya katiba kuhusu mabadiliko ya uongozi endapo Rais aliyoko madarakani aidha atafariki au kwa sababu nyingine atashindwa kuendelea na majukumu yake ya Urais.

Kwetu sisi Wanamtandao wa wanawake Katiba, Uongozi na Uchaguzi imetudhibitia kwamba, katiba na hasa katiba yenye mrengo wa jinsia, ikiwa ni sheria mama, inaweza kutumika kujenga nguzo imara kwenye kuwezesha mabadiliko chanya kwenye harakati za utetezi wa madai ya haki nzetu. Fursa hii itaendelea kutupa chachu ya kuendeleza madai ya kuwepo na mabadiliko ya katiba yenye mrengo wa jinsia.




**Picha**: Moja ya mikutano na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyogusa Uwajibikaji wa Uongozi kujenga Kizazi cha Usawa na Jinsia.

02

Kuongezeka kwa idadi ya mitandao na asasi zilizojiunga na Mtandao huu wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi kumepelekea kuimarisha nguvu za matandao za utetezi na uchechemuzi wa ajenda zetu. Wngi wetu sambamba na ajenda moja ndiyo nguzo kuu ya nguvu zetu katika kuchochea na kudai mabadiliko chana.

03

Kuwepo, kukua na kuimarika kwa Mfuko wa ufadhili wa Wanawake Tanzania ni fanikio kubwa kwa Tapo la Utetezi wa Haki za wanawake na wasichana Mfuko huu umewezesha /kuchangia kuimarika kwa Tapo la utetezi wa haki za wanawake kwa njia kadhaa.

Aidha Mfuko umefadhili mashirika yanayotetea haki za wanawake katika ngazi ya taifa na ya kijamii. Mfuko umewezesha kuanzishwa au kukua kwa mashirika yanaoyotetea haki za wanawake na washichana. Mfuko umeshiriki katika mijadala mbalimbali ndani na nje inayohoji mifumo ya ufadhili ambayo haiwafikii wanawake hususan watetezi wa haki za wanawake na washichana. (finacing ecosystem)`

04

Mtandao umezalisha majadiliiano rika (intergenerational dialogue) kwa kuwezesha kuwepo kwa jukwaala kujifunza kutoka rika moja na rika linguine katika kukuza maarifa na uelewa wa pamoja wa ajenda tunayoitetea.

05

Mwisho na siyo kwa daraja, Mtandao umejenga utamaduni wa kutafakari kwa kina, kujifunza na hata kusherekea mafanikio yetu. Mfano Tamasha la Jinsia la Tanzania lilioongozwa na TGNP liliweza kuleta pamoja wakilishi zaidi ya elfu mbili toka sehemu zote za nchi yetu. Vile vile sherehe za miaka 15 za Mfuko wa Ufadhili uliweza kuleta zaidi ya washiriki --- ambao kwa muda wa siku chache, walisherekea, walitafakari safari yetu na hatimaye kupendekeza maeneo ya kuimarisha.




**Picha**: Moja ya matamasha ya Jinsia yanayochochea uongozi wa wanawake, usawa wa Jinsia na upingaji wa ukatili

## 3.2 CHANGAMOTO

Katika kiipindi cha mwongo mmoja, Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi umekutana na changamoto kadhaa ambazo zimeathiri kwa kiwango Fulani kufikia malengo yetu.

### 01

Kwanza kabisa ni kuwepo kwa mifumo kandamizi yenye kuweka vikwazo katika ujenzi wa Tapo la kifeminia. Kwa mfano wakati tulipokuwa tukidai kuingizwa Kwa masuala 12 kwenye mchakato wa katiba, wapo wenzetu ikiwa ni pamoja na asasi zinazodai kutetea haki za binadamu kuona kwamba masuala ya wanawake na watoto siyo ajenda pana kwenye mchakato wote wa kutayarisha katiba mpya.

### 02

Ufinyo wa rasililmali fedha ulilyopelekea mtandao kutegemea kufanya shughuli nyingi kwa kupitia kamati za ufundi. Pamoja na kwamba kamati za ufundi ziliongezeka kutoka kamati moja yenye watu 15 hapo awali, kufikia kamati  kamati tatu, ikiwa ni Kamati ya Mtandao waWanawake Katiba naUongozi yenye wawakilishi 20, Kamati ya Mtandao wa Kupinga Rushwa Ya Ngono yenye wawakilishi 14, Kamati ya Mtandaowa Ke Storia yenye watu watu 11, Kamati ya Mtandao wa Hakiya Afya ya Uzazi yenye watu 11. Changamoto kubwa ni uwakilishi wa asasi na mitandao ya kijamii kwenye kamati hizi.

### 03

Mfumo wa kuratibu kwa kupitia Mfuko wa ufadhili ambao kwa macho ya wengine kwenye mtandao Shughuli ya Mfuko ni kufadhili na kushiriki katika utendaji. Kwanza ieleweke kwamba, Mfuko huu wa kifeminia hauendeshwi kama mfuko wa kugawa rasilimali fedha pekee. Ni mfuko unaoshiriki katika harakati za kuleta mabadiliko ya kimapinduzi katika kutetea matumizi linganifu ya rasilimali za fedha kutokana na vyanzo mbalimbali.

Pili ieleweke kwamba kuratibu ni kazi isiyo na malipo (privilege), na kwamba uratibu ulio bebwa na mfuko ni ongezeko la mzigo wa kazi na uwajibikaji. Vile vile uratibu ulitokana na ke storia ya Mtandao wetu kwamba walikuwa wachache wetu waliojitwisha jukumu hili la kuratibu kazi nzito iliyowezwa kutufikisha hapa pamoja na changamoto nyingi zilizotupata katika safari yetu.

Hivyo tutakapotafari kutwalia mfuko jukumu hili kubwa la kubeba mzigo huu na tutakapomtwishwa mwenzetu mshiriki katika mtandao mpana, tutambue kwamba ni kazi yenye kuhitaji kujitolea kwa hali ya juu. Shughuli za uratibu zinaweza zifanywe na taasisi yoyote iliyo na utayari wa kuendesha shughuli zinazotakiwa kwenye uratibu.

### 04

Mwisho lakini siyo kwa daraja, uelewa wa ajenda ya pamoja umekuwa na changamoto na kutishia kudhoofisha jitihada za ujenzi wa Tapo imara la utetezi wa haki za wanawake.

## 3.3 Mfunzo Yatokanayo na Safari Yetu

Funzo moja kubwa litokanalo la mafanikio na changamoto ni : Umoja wetu, sauti zetu, na nguvu kubwa na ni turufu ya mabadiliko tunayotaka kuyaleta.

> **Umoja wetu, sauti zetu, na nguvu kubwa na ni turufu ya mabadiliko tunayotaka kuyaleta.**

## 3.4 Matarajio Yetu Yatokanayo na mafunzo ya Safari yetu.

Huu ni mjadala endelevu tutaendelea kujihoji, sisi ni nani? Tumetoka wapi? Tuna maono yapi katika kujenga Nchi yetu ambayo ubaguzi wa aina yoyote utakuwa simulizi iliyopitwa na wakati.



MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI NA UONGOZI

WOMEN FUND TANZANIA TRUST
Empowering Local Women Heroes





## Contact

info@wftrust.or.tz

www.wftrust.or.tz

P. O. Box 79235
Dar es Salaam, Tanzania
17 Rufiji Street, Masaki
Dar es Salaam, Tanzania

T: +255 22 26 00 944
M: +255 753 912 130

@womenfund_tz